


Agizo la Afisa wa Afya wa Mtaa wa Kaunti ya King

Matukio ya umma yenye watu wengi, maeneo ya burudani ndani ya majengo, maeneo ya mazoezi, mikahawa, na baa lazima zitahitaji wateja/watu kuonyesha idhibati kwamba wamepokea chanjo au matokeo yanayoonyesha hawana ugonjwa wa covid-19

Septemba tarehe 16, 2021



Kuanzia oktoba tarehe 25:

Wateja/watu watahitajika kuonyesha idhibati kuwa wamepokea chanjo ya COVID-19 au matokeo yanayoonyesha hawana ugonjwa wa COVID-19 ili waruhusiwe kuingia kwa:

- **Shughuli za nje ya majengo** zenye watu mia tano au zaidi (hii ni Pamoja na michezo ya kitaalamu na ya vyuo vya elimu na shughuli za burudani)
- **Shughuli za burudani za ndani ya majengo au sehemu za biashara** (hii ni Pamoja na michezo ya kitaalamu na ya vyuo vya elimu, burudani, maigizo ya kisanaa, ukumbi wa maigizo, muziki unaochezwa moja kwa moja, maeneo ya mazoezi na mikutano)
- **Mikahawa na baa** (hii ni Pamoja na maeneno ya ndani ya majengo ya watu kulia chakula). Hii haitumiki kwa maeneo ya nje ya majengo ya watu kulia

Kuanzia disemba tarehe 6:

Wateja/watu watahitajika kuonyesha idhibati kuwa wamepokea chanjo ya COVID-19 au matokeo yanayoonyesha hawana ugonjwa wa COVID-19 ili waruhusiwe kuingia kwa:

- **Mikahawa na baa** ambazo zina idadi ya watu kumi na wawili au chini yake



Ni nini inazingatiwa kama idhibati kuwa umepokea chanjo?

- Kadi ya chanjo ya CDC au picha ya kadi ya chanjo
- Stakabadhi kutoka kwa rekodi za matibabu / mtoa huduma ya chanjo
- Idhibati kuwa umepokea chanjo kutoka kwa jimbo au nchi nyingine
- Programu za rununu kutoka kwa watoa huduma wa afya (zilizoidhinishwa na idara ya afya ya WA)
- Cheti kilichochapiswa au nambari/kodi ya QR (itapatikana mwisho wa mwezi wa Septemba) kutoka kwa tovuti ya MyIRMobile.com

Huhitaji kuonyesha kitambulisho Pamoja na idhibati ya kuwa umepokea chanjo.

Rununu ya MyIR ni nini?

Rununu ya MyIR ni ukurasa wa mtandao unaowapatia watu uwezo wa kuangalia rekodi rasmi za Jimbo kuhusu chanjo.

Unaweza kufungua akaunti kwa tovuti ya

www.MyIRMobile.com

Rununu ya MyIR kwa sasa inapatikana kwa lugha ya Kiingereza pekee. Kwa usaidizi wa lugha, au usaidizi wa ziada wa jinsi ya kupata rekodi zako, piga simu kwa nambari ya usaidizi ya chanjo ya

Jimbo la Washington kwa nambari (833) 829-4357 au tuma

baruapepe kwa waisrecords@doh.wa.gov

Ikiwa hujapokea chanjo au huwezi kuthibitisha hali yako ya chanjo, basi lazima uonyeshe idhibati kuwa huna ugonjwa wa COVID-19 kutoka kwa vipimo vinavyotafuta nyenzo ya maumbile kutoka kwa virusi vya Corona (PCR) iliyofanywa masaa sabini na mawili yaliyopita, au matokeo ya haraka yanayoonyesha huna COVID-19 kutoka kwa mtoa huduma wa vipimo iliyofanywa papo hapo katika hafla/shughuli au majengo ya biashara kabla tu ya kuingia.



Kwa habari zaidi, tembelea tovuti ya

kingcounty.gov/verify

Public Health
Seattle & King County

